Mlisheni mwenye njaa, na mtembeleeni mgonjwa, na mwacheni huru mateka

Imepokewa kutoka kwa Abuu Mussa Al-Ash'ary -radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Mlisheni mwenye njaa, na mtembeleeni mgonjwa, na mwacheni huru mateka".

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Amebainisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa katika haki za Muislamu kwa ndugu yake Muislamu ni kumlisha mwenye njaa na kumtembelea mgonjwa, na kumuacha huru mateka.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/6103